

Jdg

Chapter 7

Swahili Interlinear

Reference: Swahili Biblica Neno

וַיִּשְׁכְּם וַיִּרְבְּעַל יְהוָה הוּא גִדְעוֹן וְכָל-הָעָם אֲשֶׁר 1
na-alipoamka-mapema Yerub-Baali yeye Gideoni na-wote-wa- watu waliokuwa
[H7925](#) [H3378](#) [H1931](#) [H1439](#) [H3605](#)

אֶתּוֹ וַיִּחַנּוּ עַל-חֶרְדֵּיִן וּמִחְנֵה מִדְיָן 2
pamoja-naye na-wakapiga-kambi karibu-na- Chemchemi-ya-Harodi na-kambi-ya Midiani
[H0854](#) [H2583](#) [H5878](#) [H4264](#) [H4080](#)

הָיְהוּהָ לָּו מִצְפּוֹן מִנְבֶּעֶת הַמּוֹרָה בְּעַמְקִים: 3
ilikuwa- kwake kaskazini kutoka-kilima-cha More bondeni
[H1961](#) [H6828](#) [H1389](#) [H4176](#) [H6010](#)

Ndipo Yerub-Baali (yaani Gideoni) na lile jeshi lililokuwa pamoja naye, wakaondoka asubuhi na mapema na kupiga kambi kando ya chemchemi ya Harodi. Kambi ya Wamidiani ilikuwa kaskazini yao katika bonde karibu na kilima cha More.

וַיֹּאמֶר יְהוָה אֶל-גִּדְעוֹן רַב הָעָם אֲשֶׁר מִתְנִי 2
na-akasema Yahwe kwa- Gideoni wengi watu walioko pamoja-nawe kutoa-kwangu
[H0559](#) [H3068](#) [H0413](#) [H1439](#) [H0854](#) [H5414](#)

אֶת-מִדְיָן מִכּוֹן-וָאֵל מִיִּכְוֹן אֲשֶׁר עַל-יִשְׂרָאֵל לְאֹמֶר יְדִי 3
Midiani - mikononi-mwao asije- akajisifu dhidi-yangu Israeli kusema mkono-wangu
[H4080](#) [H0853](#) [H3027](#) [H6435](#) [H3478](#) [H0559](#) [H3027](#)

הוֹשִׁיעָה לִּי: מְוֵנְיֶוּעַ 4
umeniokoa mwenyewe
[H3467](#)

Bwana akamwambia Gideoni, "Jeshi lililo pamoja nawe ni kubwa sana kwa mimi kuwatia Wamidiani mikononi mwao. Ili kwamba Israeli asije akajisifu juu yangu akisema, 'Mkono wangu ndio ulioniokoa,

וַעֲתָה וְעָזְרָה נָא בְּאֵזְנֵי הָעָם לְאֹמֶר מִי-אֲנֹגוֹפָא 3
na-sasa tangaza tafadhali masakioni-mwa kusema yeyote-ambaye- anaogopa
[H6258](#) [H7121](#) [H4994](#) [H0241](#) [H0559](#) [H4310](#) [H3373](#)

וְחָרָד וְיִשָּׁב וַיִּצְפֹּר מִתֵּר הַגִּלְעָד וַיִּשָּׁב מִן- 4
na-anatetemeka arudi na-aondoke kutoka-Mlima-wa Gileadi na-wakarudi kutoka-kwa-
[H2730](#) [H7725](#) [H6852](#) [H2022](#) [H1568](#) [H7725](#)

הָעָם עֹשְׂרִים וּשְׁנַיִם אֵלְף וְעֶשְׂרֵת אֵלְפִים נִשְׂאָרוּ: 5
ishirini watu na-mbili elfu elfu kumi walibaki
[H6242](#) [H8147](#) [H0505](#) [H6235](#) [H0505](#) [H7604](#)

kwa hiyo sasa tangaza jeshi lote likiwa linasikia, kwamba: Yeyote anayeogopa na kutetemeka, yeye na arudi nyumbani, aondoke katika Mlima Gileadi." Hivyo watu 22,000 walirudi, wakabaki 10,000.

4
 וַיֹּאמֶר יְהוָה אֶל-גִּדְעוֹן עוֹדֵי הָעָם רַב הוֹרֵר אוֹתָם אֶל-
 na-akasema Yahwe Gideoni bado watu ni-wengi walete-chini wao kwa-
[H0559](#) [H3068](#) [H0413](#) [H5750](#) [H1439](#) [H0413](#)

הַמַּיִם וְאֶצְרַפְנוּ לָךְ שָׁם וְהָיָה אֲשֶׁר־אָמַר אֵלֶיךָ וְהָיָה
 maji na-nitawapima kwako huko na-itakuwa yeyote-ambaye nitamwambia wewe huyu
[H4325](#) [H6884](#) [H8033](#) [H1961](#) [H0559](#) [H0413](#) [H2088](#)

יִלְךְ אַתָּה וְהָיָה עִמָּךְ יִלְךְ אַתָּה וְכֹל אֲשֶׁר-אָמַר אֵלֶיךָ
 ataenda pamoja-nawe yeye ataenda pamoja-nawe na-kila ambaye-nawe wewe
[H3212](#) [H0854](#) [H1931](#) [H3212](#) [H0854](#) [H0413](#) [H0559](#)

וְהָיָה לֹא-יִלְךְ עִמָּךְ הוּא לֹא יִלְךְ:
 hata yeye pamoja-nawe ende asi huyu
[H3212](#) [H3808](#) [H1931](#) [H3212](#) [H3808](#) [H2088](#)

Lakini Bwana akamwambia Gideoni, "Idadi ya jeshi bado ni kubwa. Wapeleke chini katika maji nami nitawajaribu huko kwa ajili yako. Kama nikikuambia, 'Huyu atakwenda pamoja nawe,' yeye atakwenda; lakini kama nikisema, 'Huyu hatakwenda pamoja nawe,' yeye hatakwenda."

5
 וַיִּזְרַד אֶת-הָעָם אֶל-יְהוָה וַיֹּאמֶר יְהוָה אֶל-גִּדְעוֹן
 na-akawaleta-chini - watu maji kwa-
[H3381](#) [H0853](#) [H0413](#) [H3068](#) [H0559](#) [H1439](#)

כֹּל אֲשֶׁר-יִלְךְ בְּלִשְׁוֹנוֹ מִן-הַמַּיִם כַּאֲשֶׁר יִלְךְ
 kila atakayeramba- atakayeramba- kwa-ulimi-wake kutoka-maji kama anavyoramba
[H3605](#) [H3952](#) [H3956](#) [H4325](#) [H3952](#) [H1290](#)

הַכֶּלֶב תִּצְיֵן אוֹתוֹ לְכֹד וְכֹל אֲשֶׁר-יִכְרַע עַל-בְּרִיכּוֹ
 mweke yeye peke-yake na-kila atakaye- piga-magoti juu-ya- magoti-yake
[H3611](#) [H3322](#) [H0853](#) [H0905](#) [H3605](#) [H3766](#) [H1290](#)

לְשֵׁתוֹת:
 kunywa
[H8354](#)

Hivyo Gideoni akalileta lile jeshi chini kwenye maji naye Bwana akamwambia Gideoni, "Watenge upande mmoja wale wote wanywao maji kwa ulimi, kama vile mbwa anywavyo, wale wote wapigao magoti ili kunywa wakipeleka mikono yao vinywani mwao, waweke upande mwingine."

6
 וַיְהִי מִסְפָּר הַמְּלַקְקִים אֶל-בֵּידֵם שְׁלֹשׁ מֵאוֹת אִישׁ
 na-ikawa hesabu-ya walioramba kwa- kwa-mikono-yao vinywa-vyao mia tatu watu
[H1961](#) [H4557](#) [H3952](#) [H3027](#) [H6310](#) [H7969](#) [H3967](#) [H0376](#) [H0413](#)

וְכֹל יֵתֵר הָעָם כָּרְעוּ עַל-בְּרִיכְיָם לְשֵׁתוֹת מַיִם:
 na-wote waliobaki-wa watu walipiga-magoti juu-ya- magoti-yao kunywa
[H3605](#) [H3766](#) [H1290](#) [H8354](#) [H4325](#)

Idadi ya wale waliokunywa kwa kuramba ramba walikuwa 300, lakini wengine wote katika jeshi walipiga magoti ili kunywa.

7
 וַיֹּאמֶר יְהוָה אֶל-גִּדְעוֹן בְּשֵׁלֶשׁ מֵאוֹת הָאִישׁ הַמְּלַקְקִים אוֹשִׁיעַ אֶתְכֶם
 na-akasema Yahwe Gideoni kwa- kwa-mia watu tatu walioramba nitawaokoa ninyi
[H0559](#) [H3068](#) [H0413](#) [H1439](#) [H7969](#) [H3967](#) [H0376](#) [H3952](#) [H3467](#) [H0853](#)

וְנִתְּתִי אֶת-מִדְיָן וְכֹל-הָעָם יִלְכוּ אִישׁ
 na-nitamtia - Midiani mkononi-mwako na-wote-wa- watu waende kila-mtu
[H5414](#) [H0853](#) [H4080](#) [H3027](#) [H3605](#) [H3212](#) [H0376](#)

לְמַקְמוֹ:
 mahali-pake
[H4725](#)

Bwana akamwambia Gideoni, “Kwa hao watu 300 walioramba maji nitawaokoa ninyi, nami nitawatia Wamidiani mkononi mwako. Waache hao watu wengine wote warudi kila mmoja nyumbani mwake.”

וַיִּקְחוּ	אֶת־	צָרָה	הָעָם	בְּיָדָם	וְאֵת	שׁוֹפְרֵי־תְּיָהֶם	וְאֵת		8
na-	-	chakula-cha	watu	mikononi-mwao	na-	tarumbeta-zao			
H3947	H0853	H6720		H3027	H0853	H7782	H0853		
כָּל־	אִישׁ	יִשְׂרָאֵל	שָׁלַח	אִישׁ	לְאֶהֱלָיו	וּבְשָׁלֶשׁ-	מֵאוֹת	הָאִישׁ	
watu-wote-wa	mtu	Israeli	aliwaaga	kila-mtu	hemani-mwake	na-kwa-mia-	tatu	watu	
H3605	H0376	H3478	H7971	H0376	H0168	H7969	H3967	H0376	
הַחֹזֵק	וּמְחַנְהָ	מִדְּוָן	הָיָה	לּוֹ	מִתַּחַת	בְּעֵמֶק:	בְּ		
aliwashika	na-kambi-ya	Midiani	ilikuwa	kwake	chini-yake	bondeni	ᵑ		
H2388	H4264	H4080	H1961		H8478	H6010			

Hivyo Gideoni akawaacha wale Waisraeli wengine kila mmoja aende kwenye hema yake. Akabakia na wale 300, ambao walichukua vyakula na tarumbeta za wale wenzao. Basi kambi ya Wamidiani ilikuwa chini yake bondeni.

וַיְהִי	בְּלַיְלָה	הַהוּא	וַיֹּאמֶר	אֵלָיו	יְהוָה	קוֹם	רָד	בְּמַחֲנֶה	כִּי	9
na-ikawa	usiku	ule	na-akamwambia	yeye	Yahwe	simama	shuka	kambini	kwa-kuwa	
H1961	H3915	H1931	H0559	H0413	H3068		H3381	H4264		
נִמְעִיתָ	בְּיַדְּךָ:									
nimeitia	mkononi-mwako									
H5414	H3027									

Usiku ule ule Bwana akamwambia Gideoni, “Ondoka, ushuke kambini, kwa kuwa nimeitia mkononi mwako.

וְאֵם־	יָרָא	אֶתָּה	לְקַדְדָת	רָד	אֶתָּה	וּפְרָה	נַעֲרֶךָ	אֶל־	10
na-ikiwa-	unaogopa	wewe	kushuka	shuka	wewe	na-Pura	mtumishi-wako	kwa-	
	H3373		H3381	H3381		H6513	H5288	H0413	
הַמַּחֲנֶה:									
kambi									
H4264									

Lakini kama unaogopa kushambulia, shuka kambini pamoja na mtumishi wako Pura,

וּשְׁמַעְתָּ	מֵה־	יִדְבְּרוּ	וְאַחַר	הַחֲזִיקְנָה	יְדִיךָ	וַיְרִדְתָּ	בְּמַחֲנֶה		11
na-utasikia	nini-	wanasema	na-baadaye	zitaimarishwa	mikono-yako	na-utashuka	kambini		
H8085	H4100	H1696		H2388	H3027	H3381	H4264		
וַיִּרְדַּ	הוּא	וּפְרָה	נַעֲרוֹ	אֶל־	קָצָה	הַחֲמִשִּׁים	אֲשֶׁר		
na-akashuka	yeye	na-Pura	mtumishi-wake	kwa-	ncha-ya	waliojipanga-kwa-vita	waliokuwa		
H3381	H1931	H6513	H5288	H0413		H2571			
הַמַּחֲנֶה:									
kambini									
H4264									

nawe sikiliza wanayosema. Hatimaye, utatiwa moyo kushambulia kambini.” Basi yeye na Pura mtumishi wake wakashuka na kufikia walinzi wa mbele wenye silaha waliokuwa mle kambini.

בְּעֵמֶק bondeni H6010	נִפְלִים walikuwa-wamelala H5307	מְשָׂרִיקִים mashariki	בְּנֵי- wana-wa-	וְכָל- na-wote-wa- H3605	וַעֲמֵלֵק na-Amaleki H6002	וּמִדְיָן na-Midiani H4080	12
שְׁעַל- ulio-juu-ya-	כְּחֹל kama-mchanga H2344	מְסַפֵּר hesabu H4557	אֵין hapakuwa-na H0369	וְלִנְמִלֵּיהֶם na-ngamia-zao H1581	לְרֹב kwa-wingi H7230	כְּאֶרְבָּה kama-nzige H0697	
					לְרֹב: kwa-wingi H7230	הַיָּם bahari H3220	שֹׁפֵת ufuo-wa H8193

Wamidiani, Waamaleki na mataifa mengine yote ya mashariki walikaa bondeni, nao walikuwa mfano wa nzige kwa wingi wao. Ngamia zao hazikuhesabika, wingi wao ulikuwa kama mchanga wa ufuoni mwa bahari.

הִנָּה tazama H2009	וַיֹּאמֶר na-akasema H0559	חֲלוֹם ndoto H2472	לְרֵעֵהוּ mwenzake H7453	מְסַפֵּר akimwambia	אִישׁ mtu H0376	וְהִנָּה- na-tazama- H2009	גִּדְעוֹן Gideoni H1439	וַיָּבֵא na-akafika H0935	13
בְּמִתְנָה katika-kambi-ya H4264	מִתְהַפֵּד ukiviringika H2015	שְׁעִירִים shayiri H8184	לְחֶם mkate H3899	(צָלִיל) (mkate-wa) H6742	[צָלוּל] [mkate] H6742	וְהִנָּה na-tazama H2009	חֲלִמְתִּי niliota	חֲלוֹם ndoto H2472	
לְמַעַלָּה juu H4605	וַיִּתְהַפְּקֵהוּ na-ukalipindua H2015	וַיִּפֹּל na-likaanguka H5307	וַיִּכְהֹוּ na-ukalipiga H5221	הָאֵהָל hema H0168	עַד- hadi- H5704	וַיָּבֵא na-ukafika H0935	מִדְיָן Midiani H4080		
						הָאֵהָל: hema H0168	וַיִּפֹּל na-likaanguka H5307		

Gideoni alifika wakati huo huo kukiwa na mtu mmoja aliyekuwa anamweleza mwenzake ndoto yake, akisema, "Niliota ndoto: Tazama mkate wa shayiri ulioviringana ulianguka katika kambi moja ya Wamidiani, ukaipiga na ikaanguka nao ukaipindua juu chini na hema ikaiporomoka chini."

חֲרָב upanga-wa H2719	אִם- isipokuwa-	בְּלִתִּי isipokuwa H1115	זֹאת hii H2063	אֵין si-kitu-kingine H0369	וַיֹּאמֶר na-akasema H0559	רֵעֵהוּ mwenzake H7453	וַיַּעַן na-akajibu	14
אֶת- -	בְּיָדוֹ mkononi-mwake H3027	הָאֱלֹהִים Mungu H0430	נָתַן ametoa H5414	יִשְׂרָאֵל Israeli H3478	אִישׁ mtu-wa H0376	יּוֹאֵשׁ Yoashi H3101	בֶּן- mwana-wa- H1439	גִּדְעוֹן Gideoni H1439
					כָּל- kambi H4264	הַמִּתְנָה: kambi-yote H3605	וְאֶת- na- H0853	מִדְיָן Midiani H4080

Rafiki yake akamjibu, "Habari hii si kitu kingine zaidi ya upanga wa Gideoni mwana wa Yoashi, Mwisraeli. Mungu amewatia Wamidiani na jeshi lote mkononi mwake."

וַיִּשְׁתַּחֲוּ na-akasujudu H7812	שִׁבְרוֹ tafsiri-yake H7667	וְאֶת- na- H0853	חֲתָלוֹם ndoto H2472	מְסַפֵּר maelezo-ya H4557	אֶת- - H0853	גִּדְעוֹן Gideoni H1439	כְּשֹׁמֵעַ aliposikia H8085	וַיְהִי na-ikawa H1961	15
יְהוָה Yahwe H3068	נָתַן ametoa H5414	כִּי- kwa-kuwa- H0853	קִוְמוּ simameni	וַיֹּאמֶר na-akasema H0559	יִשְׂרָאֵל Israeli H3478	מִתְנָה kambi-ya H4264	אֶל- kwa- H0413	וַיִּשָּׁב na-akarudi H7725	
					מִדְיָן: Midiani H4080	מִתְנָה kambi-ya H4264	אֶת- - H0853	בְּיַדְכֶם mikononi-mwenu H3027	

Gideoni alipoisikia hiyo ndoto na tafsiri yake, akamwabudu Mungu. Akarudi kwenye kambi ya Israeli na kusema, "Inukeni! Bwana amelitia jeshi la Wamidiani mikononi mwenu."

וַיִּחַן	אֶת־	שְׁלֹשׁ-	מֵאוֹת	הָאִישׁ	שְׁלֹשָׁה	רְאשִׁים	וַיִּתֵּן	שׁוֹפְרוֹת	16
na-akawagawanya	-	mia-	tatu	watu	vikundi	vitatu	na-akawapa	tarumbeta	
H2673	H0853	H7969	H3967	H0376	H7969	H5414	H7782		
בִּיד־	כָּל־	וּכְרִים	רְקִים	וְלִפְדִים	בְּתוֹךְ	תְּכָדִים:			
mikononi-mwa-	wote	na-mitungi	mitupu	na-mienge	ndani-ya	mitungi			
H3027	H3605	H3537	H7386	H3940	H8432	H3537			

Akawagawa wale watu 300 katika makundi matatu, akawakabidhi tarumbeta mikononi mwao wote na mitungi isiyokuwa na maji yenye mienge ndani yake.

וַיֹּאמֶר	אֵלֵיהֶם	מִמֵּנִי	תֵּרָאוּ	וְכֵן	תַּעֲשׂוּ	וַהֲגִהָ	אֲנֹכִי	17
na-akawaambia	wao	kutoka-kwangu	angalieni	na-hivyo	fanyeni	na-tazama	mimi	
H0559	H0413		H7200			H2009	H0595	
בָּא	בְּקֶצֶה	הַמַּחֲנֶה	וַהֲיָה	כְּאֲשֶׁר-	אֶעֱשֶׂה	כֵּן	תַּעֲשׂוּן:	
ninakuja	nchani-mwa	kambi	na-itakuwa	kama-nifanyavyo-	nitafanya	hivyo	fanyeni	
H0935	H4264	H1961						

Akawaambia, "Nitazameni, fanyeni kama nitakavyofanya, nitakapofika mwisho wa kambi mfanye kama nitakavyofanya.

וַתִּקְעֵתִי	בְּשׁוֹפֵר	אֲנֹכִי	וְכָל־	אֲשֶׁר	אֲתִי	וַתִּקְעֵתֶם	בְּשׁוֹפְרוֹת	18
na-nitapiga	tarumbeta	mimi	na-wote-wa-	ambao	pamoja-nami	na-mpige	tarumbeta	
H8628	H7782	H0595	H3605		H0854	H8628	H7782	
גַּם־	אֲתֶם	סְבִיבוֹת	כָּל־	הַמַּחֲנֶה	וַאֲמַרְתֶּם	לִיהוָה	וְלִגְדֵעֹן:	
pia-	ninyi	pande-zote-za	kambi-yote	kambi	na-mseme	kwa-Yahwe	na-kwa-Gideoni	
H1571		H5439	H3605	H4264	H0559	H3068	H1439	

Wakati mimi na wale walio pamoja nami wote, tutakapopiga tarumbeta zetu, ninyi nanyi pigeni tarumbeta pande zote za kambi na mpige kelele, mseme, 'Upanga wa Bwana na wa Gideoni.'

וַיִּבֶא	גִּדְעוֹן	וּמֵאָה-	אִישׁ	אֲשֶׁר-	אֵתוֹ	בְּקֶצֶה	הַמַּחֲנֶה	19
na-akafika	Gideoni	na-mia-	mtu	waliokuwa-	pamoja-naye	nchani-mwa	kambi	
H0935	H1439	H3967	H0376		H0854	H4264	H4264	
רֹאשׁ	הָאֲשַׁמֶּרֶת	הַתִּיכוּנָה	אֶדָּ	הַקִּימוּ	הַקֵּם	הַקִּימוּ	אֶת־	
mwanzo-wa	zamu-ya	kati	tu	walikuwa-wamewaweka	walikuwa-wamewaweka	walikuwa-wamewaweka	-	
	H0821	H8484	H0389				H0853	
הַשְּׂמֵרִים	וַיִּתְּקֵעוּ	בְּשׁוֹפְרוֹת	וַנְּפֹיץ	הַכְּרִים	אֲשֶׁר	בִּידֶם:		
walinsi	na-wakapiga	tarumbeta	na-wakavunja	mitungi	iliyokuwa	mikononi-mwao		
H8104	H8628	H7782	H3537			H3027		

Gideoni na wale watu 100 waliokuwa pamoja naye wakafika mwisho wa kambi usiku mwanzoni mwa zamu ya kati, mara tu walipokuwa wamebadili zamu. Wakapiga zile tarumbeta zao na kuvunja ile mitungi iliyokuwa mikononi mwao.

וַיִּתְּקֵנוּ	וַיִּשְׁבְּרוּ	הַכְּרִים	בְּשׁוֹפְרוֹת	הָרְאשִׁים	שְׁלֹשֶׁת	וַיִּתְּקֵנוּ	20
na-wakashika	na-wakavunja	mitungi	tarumbeta	vikundi	vikundi-vitatu	na-wakapiga	
H2388	H7665	H3537	H7782		H7969	H8628	
לְתַקֹּעַ	וּבִיד־	יְמִינָם	וּבִיד־	בְּלִפְדִים	שְׂמֹאוֹלִם	בִּיד־	
kupiga	na-kwa-mkono-wa-	kulia	na-kwa-mkono-wa-	mienge	kushoto	kwa-mkono-wa-	
H8628	H3027	H3225	H3027	H3940	H8040	H3027	
	וְלִגְדֵעֹן:	לִיהוָה	וַיִּקְרָאוּ	תִּרְב	וַיִּקְרָאוּ	וַיִּקְרָאוּ	
	na-kwa-Gideoni	kwa-Yahwe	upanga	na-wakapiga-kelele	na-wakapiga-kelele	na-wakapiga-kelele	
	H1439	H3068	H2719	H7121			

Yale makundi matatu yakapiga tarumbeta na kuvunja mitungi. Wakashika mienge kwa mikono yao ya kushoto na katika mikono yao ya kuume tarumbeta ili kuzipiga, wakapaza sauti zao, “Upanga wa Bwana na wa Gideoni!”

כָּל־ kambi-yote H3605	וַיִּרְץ na-wakakimbia H7323	לְמַחֲנֵה kambi H4264	סָבִיב pande-zote-za H5439	תַּחֲתָיו mahali-pake H8478	אִישׁ kila-mtu H0376	וַיַּעֲמְדוּ na-wakasimama H5975	21
			(וַיִּנְגְּסוּ:) (na-wakakimbia) H5127	[וַיִּנְגְּסוּ] [na-wakakimbia] H5127	וַיִּרְעִיעוּ na-wakapiga-kelele H7321	הַמַּחֲנֵה kambi H4264	

Wakasimama kila mtu mahali pake kuizunguka kambi pande zote, Wamidiani wote wakakimbia, huku wakipiga kelele.

אִישׁ kila-mtu H0376	חָרֵב upanga-wa H2719	אֵת - H0853	יְהוָה Yahwe H3068	וַיֵּשֶׁם na-akaweka H0853	הַשּׁוֹפְרוֹת tarumbeta H7782	מֵאוֹת tatu H3967	שְׁלֹשׁ mia- H7969	וַיִּתְקַעוּ na-walipopiga H8628	22
הַשְּׁטֵה־בַּיִת Beth-Shita H1029	עַד־ hadi- H5704	הַמַּחֲנֵה kambi H4264	וַיִּנְסֶה na-wakakimbia H5127	הַמַּחֲנֵה kambi H4264	וּבְכָל־ na-katika-kambi-yote H3605	בְּרַעְיָהוּ dhidi-ya-mwenzake H7453			
			עַל־ Tabathi H2888	טָבַת: karibu-na- H2888	מִחוּלָה־אֲבֵל Abeli-Mehola H0065	שֵׁפֶת־ mpaka-wa- H8193	עַד hadi H5704	צִרְרָתָה Serera H6888	

Walipozipiga zile tarumbeta 300, Bwana akafanya watu katika kambi yote kugeuziana upanga kila mmoja na mwenziwe. Jeshi likakimbia mpaka Beth-Shita kuelekea Serera hadi mpakani mwa Abel-Mehola karibu na Tabathi.

כָּל־ wote-wa- H3605	וּמִן־ na-kutoka- H0836	אֲשֶׁר Asheri H0836	וּמִן־ na-kutoka- H0836	מִנְפֹתָי kutoka-Naftali H5321	יִשְׂרָאֵל Israeli H3478	אִישׁ־ watu-wa- H0376	וַיִּצְעַק na-wakaitwa H6817	23
				מִדְיָן: Midiani H4080	אַחֲרָי baada-ya H7291	וַיִּרְדְּפוּ na-wakawafuatia H7291	מְנַשֶּׁה Manase H4519	

Watu wa Israeli wakaitwa kutoka Naftali, Asheri na Manase, wakawafuatia Wamidiani.

רְדִי shukeni H3381	לְאֵמֶר kusema H0559	אֶפְרַיִם Efraimu H0669	הָרִ Mlima-wa H2022	בְּכָל־ katika-wote-wa- H3605	גִּדְעוֹן Gideoni H1439	שָׁלַח alituma H7971	וּמִלְאָכִים na-wajumbe H4397	24
יַרְדֵּן Yordani H3383	וְאֵת־ na- H0853	בְּרַחֲבֵיהֶם Beth-Bara H1012	עַד hadi H5704	הַמַּיִם maji H4325	אֵת־ - H0853	לְקָמוֹ kwao H3920	מִדְיָן Midiani H4080	לְקִרְאָתָם kuwalaki H7125
בְּרַחֲבֵיהֶם Beth-Bara H1012	עַד hadi H5704	הַמַּיִם maji H4325	אֵת־ - H0853	וַיִּלְכְּדוּ na-wakakamata H3920	אֶפְרַיִם Efraimu H0669	אִישׁ mtu H0376	כָּל־ watu-wote-wa H3605	וַיִּצְעַק na-wakaitwa H6817
							וְאֵת־ Yordani H3383	נָא־ na- H0853

Gideoni akatuma wajumbe katika nchi yote ya vilima vya Efraimu akisema, “Teremkeni dhidi ya Wamidiani na mkazuie vivuko vya maji mbele yao hadi Beth-Bara na pia Yordani.” Hivyo watu wote wa Efraimu wakakutanika pamoja na kuzingira mto wa Yordani hadi Beth-Bara.

זָאב	וְאֶת־	עֲרֵב	אֶת־	מִדְיָן	שָׂרִי	שָׁנִי־	וַיִּלְכְּדוּ	
Zeebu	na-	Orebu	-	Midiani	wakuu-wa	wakuu-wawili-wa-	na-wakawakamata	
H2062	H0853	H6159	H0853	H4080	H8269	H8147	H3920	
	הָרְנִי	זָאב־	וְאֶת־	עֲרֵב	בְּצֹר־	עֲרֵב	אֶת־	וַיִּתְרְנִי
	walimuua	Zeebu	na-	Orebu	kwenye-Mwamba-wa-	Orebu	-	na-wakamuua
	H2026	H2062	H0853	H6159	H6697	H6159	H0853	H2026
עֲרֵב	וְרֵאשׁ־		מִדְיָן	אֶל־	וַיְרִדְפוּ	זָאב	בְּיָקֵב־	
Orebu	na-vichwa-vya-		Midiani	kwa-	na-wakawafuatia	Zeebu	kwenye-Shinikizo-la-Divai-la-	
H6159			H4080	H0413	H7291	H2062	H3342	
				לְיִרְדָּן:	מֵעֵבֶר	גִּדְעוֹן	אֶל־	הַבְּלִיאִי
				Yordani	ng'ambo-ya	Gideoni	kwa-	walileta
				H3383	H5676	H1439	H0413	H0935
								וּזָאב
								na-Zeebu
								H2062

Wakawakamata wakuu wawili wa Midiani, Orebu na Zeebu. Wakamuulia Orebu pale penye mwamba wa Orebu, na Zeebu wakamuulia penye shinikizo la kukamulia divai la Zeebu. Wakawafuatia Wamidiani na kuleta vichwa vya Orebu na Zeebu kwa Gideoni, huko ng'ambo ya Yordani.